St. Gaspar Nursing School
P.O. BOX 12, Itigi.
Singida-Tanzania.
TEL. 0732- 960685,
Fax: 0732- 960744.
E-Mail 1: info@stgasparhopital.com
E-Mail 2: stgasparhopital@yahoo.com

Hongera kwa kufanikiwa kuchaguliwa kujiunga katika chuo cha Uuguuzi cha Mt. Gaspar. Chuo hiki kinatoa kozi ya Uuguzi. Kozi hii ni ya miaka mitatu lakini unaweza kusoma kwa miaka miwili na kuhitimu kwa ngazi ya cheti.

Chuo kipo chini ya Usimamizi wa Kanisa Katoliki kikiendeshwa na Shirika la Wamisionari wa Damu Takatifu ya Yesu. Kwa kuwa chuo kinaendeshwa na Kanisa Katoliki kinafuata maadili, kanuni na taratibu za kikatoliki. Chuo kimesajiliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii pamoja na NACTE. Chuo cha Uuguzi cha Mt. Gaspar kinapokea wanachuo wa jinsia zote (Wanaume na Wanawake).

Chuo kipo katika Mkoa wa Singida umbali wa km. 117 kutoka Singida mjini na umbali wa km. 40 kutoka Manyoni. Mazingira mazuri ya chuo na ya hospitali yanamfanya mwanachuo kuwa katika nafasi nzuri ya kusoma na hivyo kufaulu vizuri. Chuo kina kila kitu muhimu na cha lazima kwa kujisomea (walimu, majengo mazuri, vitabu, maji, vifaa vya mazoezi, umeme na hopitali nzuri). Chuo kinao uwezo wa kuchukuwa wanachuo wasiozidi 50 kwa kila kozi kila mwaka. Unakaribishwa sana katika Chuo cha Uuguzi cha Mt. Gaspar.

A: MUUNDO WA ADA KWA UP-GRADING 2020-2021

NO	MCHANGANUO	MWAKA 1
1	ADA YA MAFUNZO	1,000,000.00
2	ADA YA MALAZI	355,000.00
3	MATENGENEZO & MAENDELEO	50,000.00
4	ADA YA VITABU & MITIHANI	40,000.00
	JUMLA	1,445,000.00

B: MALIPO MENGINE YA :

NO	MCHANGANUO	MWAKA I
1	CHAKULA	1,400,000.00
2	KITAMBULISHO	10,000.00
3	MICHANGO JIMBO NA CSSC	10,000.00
		1,420,000.00

1. Ada pamoja na malipo mengine yanapaswa kulipwa mara moja mwanachuo anapoanza chuo.Malipo haya yanaweza kufanyika mara moja kwa mkupuo au mara mbili tu na si zaidi.Ukiona unapenda kulipa kwa awamu tatu lazima kuitaarifu ofisi kimaandishi juu ya mpango wako wa kulipa ada.
2. Ada na malipo mengine yanapaswa kulipwa muhula wa kwanza wa kila mwaka. Aidha kama unalipa kwa awamu mbili basi kila mwanzo wa muhula.
3. Mwanachuo hataruhusiwa kuanza muhula wa pili au kurudi nyumbani kutafuta
   Ada na malipo mengine. Hivyo unapaswa kupanga vizuri kuhusu ada na malipo mengine.
4. **Mwanachuo akiamua au akishauriwa kusitisha masomo kwasababu yoyote ile hawezi kurudishiwa ada yake pamoja na malipo mengine aliyofanya.**
5. Kwa wale wenye ***Bima ya Afya*** mara wanapofika chuoni wahakikishe wamefika na kitambulisho cha bima na kukiwasilisha kwa mkuu wa chuo ili kisajiliwe kinyume cha hilo watapaswa kulipa **TSHS 50,400.00** kwa mwaka ambazo mara baada ya kuzilipa utapewa kitambulisho cha Bima na utakuwa unatibiwa kwa Bima. Njoo na fedha hizi ili upatiwe matibabu kwa njia ya Bima usipokuja nazo hutaweza kutibiwa na hivyo hatuwezi kukupokea chuoni. Kila mwenye kadi ya bima atapaswa kutumia kadi yake ya bima kila anapokwenda kutibiwa. Fedha ya Bima ya afya italipwa kila mwaka.
6. ***(i)Malipo ya mafunzo ya vitendo ya Afya ya Jamii (Community Field) mwanachuo anapaswa kuwa na Tshs. 150,000.00 katika muhula wa kwanza wa mwaka wa pili na fedha zote hizi atakuwanazo mwenyewe na atagharamikia usafiri na muda wote atakaokuwa huko vijijini.***
   (ii)Aidha utapaswa kulipia Tshs. 15,000.00 kwa ajili ya NACTE Quality Assurance kwa Mwaka.
   (iii) Utapaswa kulipa ada ya mtihani wa Wizara Tshs. 150,000.00 kwa mwaka Fedha hii inalipwa katika akaunti ya Wizara kabla ya tarehe 30, Mei ya kila mwaka.
   (iv) Mwaka wa tatu utapaswa kugharamikia Tshs. 350,000.00 kwa ajili ya mafunzo ya vitendo ya Afya ya akili (Mental Health) kwa siku 35 huko Dodoma.
   (v) Gharama ya utafiti (Research)ni Tshs. 150,000.00 Fedha hii asipewe mtu yeyote bali abaki nayo na atadaiwa na ofisi kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na ofisi.
7. ***Ada yote kwa miaka mitatu ni Tshs 8,310,000.00. Kwa mwaka wa kwanza ni Tshs. 2,910,000.00, Mwaka wa pili Tshs. 2,700,000.00 Mwaka wa tatu ni 2,700,000.00 Lakini Ada hii inaweza kubadilika wakati wowote kutokana na mabadiliko yatakayo tokea. Na mabadiliko yatakayojitokeza yatatolewa kwa njia ya barua kutoka chuoni.***
8. Mwanachuo anaowajibu wa kujua kiasi cha fedha ya ada na malipo mengine anachodaiwa na hivyo kuhakikisha anakamilisha. Uongozi hautawajibika kwa lolote kwa mwanachuo kusimamishwa masomo au kutopewa namba ya mtihani kutokana na tatizo la kutokamilisha ada na malipo mengine.
9. **Vitabu vifuatavyo: General Nursing Experience Book vitapatikana kwa gharama ya Tshs 15,000.00, Delivery Book Tshs 25,000.00 na P.V. Book kwa Tshs. 5,000.00. Vitabu hivi ni lazima uwenavyo katika muhula wa kwanza wa mwaka wa kwanza wa masomo. Vitabu hivyo vinapatikana hapa chuoni.**

SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO

1) Tafadhali zisome kwa uangalifu na kuzielewa kisha kwa hiari yako mwenyewe kabla ya kuja chuoni usaini kuzikubali na kuzifuata.
2) Njoo chuoni na karatasi uliyosaini na kuikabidhi kwa Mkuu wa chuo.
3) Uvunjifu wa sheria hizi hupelekea adhabu au kusimamishwa masomo kwa muda na hata kufukuzwa chuo moja kwa moja

1. CHAKULA:

i. Chakula kitatolewa kulingana na muda uliopangwa na chuo.
ii. Chakula maalumu kwa mwanachuo kitatolewa kulingana na maelekezo ya daktari na baada ya kuthibitishwa na mkuu wa chuo.
iii. Hairuhusiwi chakula kutolewa nje ya chumba cha chakula isipokuwa kwa ruhusa maalumu.
iv. Ni marufuku kupika katika vyumba vya kulala na eneo la chuo. Ukigundulika utasimamishwa masomo au kufukuzwa kabisa.
v. Wageni wa wanachuo hawaruhusiwi kushiriki katika chakula cha wanachuo.
vi. Hakuna mwanachuo anayeruhusiwa kula nje ya chuo wala kuleta chakula toka nje bila ruhusa maalum.

2. SHUGHULI NYINGINEZO:

i. Kila mwanachuo lazima ashiriki kikamilifu katika michezo na shughuli nyingine zote ambazo Uongozi wa chuo umepanga **(kazi za mikono kwa ajili ya kujitegemea zinasisitizwa na ni lazima kwa kila mmoja kushiriki usiposhiriki utasimamishwa masomo au kufukuzwa chuo moja kwa moja).**

3. MUDA:

i. Wanachuo wote wanatakiwa kuwa chuoni muda wote isipokuwa kama wanafanya mazoezi ya vitendo watakuwa eneo la hospitali tu.
ii. Hairuhusiwi mwanachuo kuwa nje ya eneo la chuo bila ruhusa. Wanachuo wanaruhusiwa kutoka katika eneo la chuo kwa matembezi **mara moja tu** kwa mwezi nayo ni **Jumamosi ya mwisho wa mwezi** tu. Na Jumamosi hii itatumika kama “Banking day”. Na mwanachuo atapaswa kuwa amerudi chuoni kabla ya **saa 12:00 jioni.**
iii. Taa zote zitazimwa **saa 4:00 usiku** isipokuwa taa za nje na kwa wakati mwingine zinaweza kuchelewa kuzimwa kutokana na tukio maalumu.
iv. Wanachuo wanapaswa kurudi kutoka likizo siku iliyopangwa. Siku ya kufungua chuo kila mmoja anatakiwa afike chuoni kabla ya saa **12: 00 jioni.** Mwanachuo anayechelewa chuoni lazima aombe ruhusa ya kuchelewa kinyume na hapo hatapokelewa hata kama ni siku moja.
v. Mwanachuo anatakiwa kutumia muda wake vizuri kwa kujisomea na kwa kufanya mazoezi ya masomo.

vi. Wanachuo wanaokuwa zamu za mafunzo kazini (wards rotation) kutokana na utaratibu wa mafunzo lazima wafuate taratibu zote za chuo na hospitali. Kinyume na hivyo utaweza kusimamishwa masomo au kufukuzwa chuo.

4. NGUO:

i. Sare rasmi za chuo lazima zivaliwe na wanachuo wakati wote wakiwa kazini, hospitalini, madarasani, chuoni, na katika shughuli maalumu zitakazo tangazwa.
ii. Wanachuo wote wanapaswa kuvaa sare, na wawe wasafi wakati wote. Sare (uniform) za shule zitashonwa hapa hapa chuoni.
iii. Wakati usio wa darasa au mafunzo kwa vitendo wanachuo watavaa mavazi yao ya nyumbani yenye heshima na nidhamu. Ikionekana kuvaa mavazi yasiyo na nidhamu utachukuliwa hatua za kinidhamu.
iv. Mwanachuo aje na nguo za michezo (bukta, track– suit na viatu Vitakaguliwa).
v. Mwanachuo anapokuwa nje ya chuo ni lazima avae mavazi yenye nidhamu na heshima kama ilivyoainishwa kwenye sheria na taratibu za chuo.

5. USAFI:

i. Wanafunzi wanawajibika kwa usafi wa mabweni yao na mazingira yao.
ii. Hairuhusiwi kubandika magazeti na picha mbalimbali katika vyumba isipokuwa katika ubao wa matangazo tu.
iii. Lazima wanafunzi kuacha maeneo waliyotumia katika usafi na katika mpangilio mzuri. Kabla ya kwenda likizo lazima kukabidhi chumba kwa wadeni kikiwa safi. Ukiacha chumba na mazingira yako yakiwa machafu utalipa **Tshs. 20,000.00**
iv. Kufuga ndevu au sharafu hairuhusiwi.
v. Wasichana wanatakiwa kusuka nywele au kuchana. Lipstick, kucha ndefu au nywele za bandia haziruhusiwi wakati wa masomo na wakati wa mafunzo kazini au hospitalini.

6. WAGENI:

ii. Wageni wote wanapokelewa na kukaribishwa katika chumba cha mapumziko tu.
iii. Wageni hawaruhusiwi kuonana na wanafunzi wakati wa masomo na mafunzo kwa vitendo wodini.
iv. Iwapo mgeni anapenda kuona mazingira ya chuo, ruhusa lazima itolewe na mkuu wa chuo.
v. Wanachuo wa kiume hawaruhusiwi kuingia katika mabweni ya wasichana na kinyume chake. Wanachuo wanapaswa kuonyesha uhusiano wenye nidhamu.
vi. Wageni hawatakiwi kuwepo maeneo ya chuoni zaidi ya saa 12:00 jioni.
vii. Wageni wanapaswa kujiorodhesha majina katika kitabu cha wageni akiandika jina lake kamili, namba ya simu kama anayo, uhusiano, anuani, tarehe na muda aliofika na kuondoka.

7. VILEO:

i. Pombe hairuhusiwi katika maeneo ya chuo.
ii. Tabia ya ulevi haikubaliki katika eneo la chuo, mabwenini na wodini.
iii. Mwanachuo haruhusiwi kuwa na dawa za kulevya bila ruhusa na kwa kuwa na dawa hizi ni lazima awe ameandikiwa na daktari anayetambulika kisheria. Matumizi ya dawa za kulevya hayaruhusiwi na ikigundulika utaachishwa chuo mara moja.

8. TABIA NA TARATIBU:

i. Makelele hayaruhusiwi katika eneo la chuo, mabwenini na hospitalini.
ii. Mwanachuo anatarajiwa kuwa na tabia njema na ajiheshimu. Hairuhusiwi kujisomea wakati wa mafunzo kwa njia ya vitendo mawodini.
iii. Simu haziruhusiwi wakati wa masomo na mafunzo ya vitendo mawodini.
iv. Mwanachuo haruhusiwi kurudi nyumbani mpaka wakati wa likizo. Kama kunasababu yoyote muhimu inayomlazimu mwanachuo kurudi nyumbani au kumweleza lolote taarifa zote zipitie kwa mkuu wa chuo. Hairuhusiwi kuwasiliana naye moja kwa moja. Ruhusa itatolewa kwa mwanachuo iwapo amefiwa na wazazi, mlezi, mtoto, mume au mke basi.

9. VIFAA / SAMANI NA MAJENGO:

i. Kila mwanachuo anawajibu wa kutunza vizuri vifaa, samani na majengo ya chuo na hospitali. Vifaa vya umeme kama vile **TV, RADIO, PASI, JIKO LA UMEME,** Vifaa vya umeme vya kutengeneza nywele haviruhusiwi. Ikibainika unavyo utasimamishwa masomo au kufukuzwa kabisa.
ii. Mwanachuo haruhusiwi kumiliki silaha au kifaa chochote kinacho hatarisha usalama wake na wawenzake mabwenini.
iii. Kifaa chochote ukiharibu kutokana na uzembe au kwa makusudi utalipa.
iv. Mwanachuo akipoteza kifaa alichokabidhiwa atalipa.

10. UGONJWA:

i. Wanachuo wagonjwa watatoa taarifa kwa wadeni au mwalimu wa darasa kabla ya kwenda kutibiwa. Anapokwenda kutibiwa lazima awe na cheti maalum na akimaliza kutibiwa anapaswa kukirudisha cheti kwa mkuu wa chuo au wadeni au mwalimu wa darasa.
ii. Hakuna mwanachuo anayeruhusiwa kumwona daktari kwa matibabu bila cheti cha matibabu kutoka kwa wadeni, au mwalimu wa darasa isipokuwa kama ni kwa dharura tu.
iii. Mwanachuo haruhusiwi kutohudhuria darasani au wodini bila ya ruhusa kwa sababu ya ugonjwa. Ili usishiriki katika shughuli za chuo au hospitali kwa sababu ya ugonjwa ni lazima upate ruhusa kutoka kwa daktari na kuthibitishwa na mkuu wa chuo.
iv. Mwanachuo akipewa rufaa kwa ajili ya matibabu, Chuo hakihusiki kumsafirisha kumpeleka kwa matibabu yake wala hakitagharamikia matibabu yake. Mzazi/Mlezi au mwajiri wake atapaswa kushughulikia.
v. Endapo kwa bahati mbaya mwanachuo atafariki akiwa chuoni gharama za maziko au kusafirisha ni jukumu la mzazi/mlezi/mwajiri.

11. UVUTAJI SIGARA:

i. Hakuna mwanachuo anayeruhusiwa kuvuta sigara wakati wa kazi aidha hospitalini wala chuoni.
ii. Mwanachuo haruhusiwi kuwa na dawa zisizoruhusiwa na zisizo na maelezo yoyote.

12. UTORO:

i. Wanachuo wote lazima wawepo na kuwahi katika shughuli zote zinazohusiana na chuo na lazima wawepo muda wote wa shughuli hizo.
ii. Haruhusiwi mwanachuo kutoroka chuoni. Mwanachuo anayependa Kusitisha masomo lazima aandike barua kwa mkuu wa chuo.
iii. Unaweza kupewa ruhusa ya kutoka nje ya chuo lakini ruhusa hii itatolewa ikiombwa kimaandishi na ukitoa sababu. Ni lazima iwasilishwe kwa mkuu wa chuo na aikubali.
iv. Ruhusa za mara kwa mara na zisizo na sababu ya msingi hazitapokelewa wala kukubalika.
v. Mwanachuo anayesitisha au asiye hudhuria darasani kwa siku 20 mfululizo katika muhula wa masomo hawezi kuendelea na masomo. Aidha mwanachuo asiye hudhuria darasani kwa siku 20 mfululizo katika muhula kutokana na ugonjwa atarudia muhula huo..

13. UJAUZITO:

i. Mwanachuo aliyemjamzito haruhusiwi kuendelea na masomo.
ii. Marufuku kwa mwanachuo wa kiume kumpa mimba mwanachuo wa kike. Hairuhusiwi kutoa mimba na ikigundulika utaachishwa masomo mara moja.
iii. Kwa mwanachuo aliyefunga ndoa kisheria na kupata ujauzito katika ndoa yake anaweza kusitisha masomo yake baada ya kuutaarifu uongozi kimaandishi juu ya hali yake na atarudi kuendelea na masomo baada ya kujifungua na baada ya bodi ya chuo kupitia ombi lake ya chuo kupitia ombi lake na kuzingatia mwongozo wa mafunzo ya Wizara ya Afya. Kwa mwanachuo asiye na ndoa kisheria akipata ujauzito atasitisha masomo na hatapokelewa tena chuoni hata akishajifungua.
iv. Mahusiano ya kimapenzi hayaruhusiwi chuoni, mabwenini na hospitalini.
v. Mwanchuo hataruhusiwa kujiunga na chuo akiwa mjamzito. Na kama itagundulika kuwa na mimba mara baada ya kujiunga ataachishwa masomo.
vi. Mwanafunzi akipata ujauzito akiwa chuoni chuo hakitahusika na mwanachuo katika suala la kumgaramikia kurejea nyumbani kwao. Mzazi/Mlezi au mwajiri wake atapaswa kubeba jukumu hilo.

14. WIZI / LUGHA CHAFU / MGOMO:

i. Migomo, lugha chafu na maandamano yasiyo na kibali havikubaliki.
ii. Wizi ni marufuku.
iii. Kupigana au matusi haviruhusiwi hata kidogo.

15. DINI, SIASA NA SHUGHULI ZA KIJAMII:

i. Shughuli yoyote ya kidini, kijamii na kisiasa lazima ipate kibali cha mkuu wa chuo.
ii. Shughuli hizi haziwezi na hazipaswi hata kidogo kuingilia shughuli na ratiba za chuo na mafunzo.
iii. Shughuli za kisiasa hazikubaliwi katika mafunzo ya chuo.

16. SAFARI

i. Mwanachuo haruhusiwi kusafiri nje ya chuo bila kibali cha mkuu wa chuo.

17. MITIHANI NA KUGUSHI MITIHANI:

i. Mwanachuo lazima afuate sheria na taratibu zote za mitihani.
ii. Kugushi kwa namna yoyote ile hakukubaliki.
iii. Mwanafunzi aliyejiunga na chuo na kugundulika kuwa ana vyeti vya kugushi chuo hakitahusika wala hakitarejesha ada wala malipo mengine.
iv. Mwanachuo anapaswa kusoma kwa bidii masomo ya nadharia na vitendo. Hivyo anapaswa kufaulu kwa kiwango kinachotakiwa na Chuo pamoja na NACTE. Kushindwa kufikia kiwango husika hupelekea kurudia mitihani hata kusimamishwa masomo. Chuo hakitahusika na kusimamishwa kwa mwanachuo hivyo ada wala malipo mengine yaliyolipwa hayata rudishwa. ***Ufaulu wa chuo chetu ni kwa alama 60. Ukifeli somo moja kwa kupata alama chini 60 utarudia mtihani na ukifeli masomo matatu kwa kupata alama chini 60 utarudia mwaka na ukifeli masomo manne hutaendelea na masomo.***

NAMNA YA KUTUMA KARO:

Ada na malipomengine unapaswa kulipia kupitia Banki. Fedha taslimu haitapokelewa. Hundi itapokelewa tu baada ya kukubaliwa Banki. Tafadhali njoo na PAY IN SLIP – ya banki uliyolipia karo na kuiwasilisha katika ofisi ya malipo ya chuo ili uweze kupatiwa risiti.Fedha kwa ajili ya matumizi binafsi isiwekwe katika akaunti ya chuo kwa kuwa ukisha weka fedha kwenye akaunti ya chuo hutarejeshewa tena.

JINA LA AKAUNTI: ST. GASPAR NURSING SCHOOL
TAWI: CRDB – SINGIDA
NAMBA YA AKAUNTI: 01J1049836000
AU
JINA LA AKAUNTI: ST. GASPAR NURSING SCHOOL
TAWI: NMB– ITIGI
NAMBA YA AKAUNTI: 51910001256

KUTHIBITISHA NA KUKUBALI:

Mimi ……. nathibitisha na kukubali kuwa, nimesoma na kuelewa vizuri sheria hizi zote zinazoongoza chuo kinachoendeshwa kwa kanuni na sheria za Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), CSSC, Hospitali ya Rufaa ya St. Gaspar na za Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii . Ninaahidi kuzifuata sheria hizi. Nisipozifuata sheria hizi nakubali kuchukuliwa hatua ya kinidhamu kama kupewa adhabu, kusimamishwa masomo hata kuachishwa masomo.

Sahihi na jina la mwanafunzi ……..... mbele ya Mzazi / Mlezi / Mfadhili/Mwajiri. Tarehe ……..

Sahihi na jina la ya Mzazi / Mlezi / Mfadhili/Mwajiri ……..... Tarehe ……...